TANGAZO LA SERIKALI Na. 681 la tarehe 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA KIKULA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Kikula ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Mji wa Makambako.

*Tangazo La Serikali Na. 681 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye njia panda ya barabara ya Mbeya - Iringa (TANZAM HIGHWAY) na barabara ya kuelekea Shule ya Sekondari Juhudi kwenye alama yenye majira – nukta 702515E, 9025526N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata barabara ya Shule ya Sekondari Juhudi kwa umbali wa kilomita 0.557 hadi alama yenye majira – nukta 701957E, 9025544N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya zamani ya Iringa kwa umbali wa kilomita 0.081 hadi kwenye alama yenye majira – nukta 701973E, 9025465N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata barabara ya Shule ya Sekondari Juhudi kwa umbali wa kilomita 0.614 hadi kwenye alama yenye majira - nukta 701423E, 9025727N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wa kilomita 0.189 hadi bonde la Luligo kwenye alama yenye majira - nukta 701394 E, 9025540 N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata bonde la Luligo kwa umbali wa kilomita 1.847 hadi kwenye alama yenye majira – nukta 699766 E, 9025270 N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 2.249 kuelekea kijito cha msimu cha Mtilinzi hadi kwenye alama yenye majira – nukta 701029 E, 9027131 N; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.408 hadi kwenye chanzo cha kijito cha msimu cha Mtilinzi kwenye alama yenye majira – nukta 701417 E, 9027002 N; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa kufuata njia panda ya barabara ya Itengelo na barabara ya zamani ya Iringa kwa umbali wa kilomita 0.417 hadi kwenye alama yenye majira – nukta 701823 E, 9026905 N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata barabara ya zamani ya Iringa kwa umbali wa kilomita 0.912 hadi kwenye alama yenye majira – nukta 702151 E, 9027757 N; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa kufuata barabara iliyopo kwa umbali wa kilomita 1.089 hadi barabara ya Mbeya – Iringa kwenye alama yenye majira – nukta 703005 E, 9027154 N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa kufuata eneo oevu kwa umbali wa kilomita 1.264 hadi Bomba la TAZAMA kwenye alama yenye majira – nukta 703557 E, 9026015 N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kufuata Bomba la TAZAMA kwa umbali wa kilomita 0.970 hadi kwenye alama yenye majira – nukta 703080 E, 9025170 N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata barabara iliyopo kwa umbali wa kilomita 0.683 hadi ulipoanzia".

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*